OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI WA TARIME

SHULE YA SEKONDARI TURWA,
S. L.P 339,
TARIME.

13/12/2021

Kumb. Na: HMT/TRW/SS/J.I/2022/

Jina la Mwanafunzi: _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI TURWA MWAKA 2022.

1:0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukutarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika **SHULE YA SEKONDARI TURWA**. **HONGERA SANA**.

Shule ya Sekondari TURWA ipo umbali wa km 1.5 Mashariki mwa Mji wa Tarime KARIBU NA SOKO LA REBU kutoka kituo kikuu cha mabasi. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **17.01.2022**. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **17.01.2022** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **31.01.2022.**

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

2.1.1 WASICHANA

i. Shati mbili za mikono mifupi zisibane kuonyesha nguo za ndani, ziwe na mfuko mmoja tu upande wa kushoto wenye nembo ya shule (utaratibu wa kupata nembo ya shule utafahamishwa siku ya kuripoti) na ziwe ndefu na zenye kuweza kuchomekewa vizuri.
ii. Sketi mbili za **RANGI YA CHUNGWA (ORANGE)** kitambaa cha suti **(Istimu namba 1).** Sketi iwe na rinda boksi moja mbele lenye ukubwa wa inchi sita, moja nyuma lenye ukubwa wa inchi sita, mawili kushoto na mawili kulia ukubwa wa inchi mbli kila moja, mkanda wa sketi uwe na upana wa inchi mbili. Sketi inatakiwa iwe ndefu kufika karibu na enka (kifundo cha mguu).
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi, vinavyofunika miguu, na vyenye kufungwa kwa kamba.
iv. Soksi nyeupe ndefu aina ya stockings, zisizo na mapambo ya aina yoyote.
v. T-shirt ya shule mikono mifupi yenye nembo ya shule (utaratibu wa kuipata utafahamishwa siku ya kuripoti).
vi. Tai mbili za rangi ya ***chungwa (orange)*** zenye nembo ya shule (utaratibu wa kuwekewa nembo utaupata siku ya kuripoti).

2.1.2 **WAVULANA**

i. Shati mbili za mikono mifupi zisibane kuonyesha nguo za ndani, ziwe na mfuko mmoja tu upande wa kushoto wenye nembo ya shule (utaratibu wa kupata nembo ya Shule utafahamishwa siku ya kuripoti) na ziwe ndefu na zenye kuweza kuchomekewa vizuri.
ii. Suruali mbili za **RANGI YA CHUNGWA (ORANGE)** kitambaa cha suti **(Istimu namba 1).** Suruali hizo zishonwe kwa staha, iwe na luksi sita, marinda mawili upande wa kushoto na kulia, mkunjo (turn up) sehemu ya miguuni na mzunguko wa mguu kwa chini usipungue nchi 18. Suruali mtindo wa **"MODO"** hazitakiwi shuleni.
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi, vinavyofunika miguu vyenye kufungwa kwa kamba.
iv. T-shirt ya shule mikono mifupi yenye nembo ya shule (utaratibu wa kuipata utafahamishwa siku ya kuripoti).
v. Tai mbili za rangi ya ***chungwa (orange)*** zenye nembo ya shule (utaratibu wa kuwekewa nembo utaupata siku ya kuripoti).
vi. Soksi nyeupe zisizo na mapambo ya aina yoyote.
vii. Mkanda mweusi wa ngozi.

2.2 MAHITAJI MENGINE

KWA WASICHANA NA WAVULANA

(i) Uwe na begi la kuhifadhia madaftari **"school bag"**. Mifuko yenye picha za wasanii hairuhusiwi.
(ii) Sweta la rangi ya **NYEUSI** lenye shingo la **V.**
(iv) Mkebe wa hesabu (Mathematical Set), rula, kalamu na Dictionary.
(v) Madaftari makubwa (Counter Books) kumi na moja (11) na madaftari madogo (Msomi) matano.
(vi) Nguo za michezo (track suit) rangi ya kijani kibichi (green) na raba za michezo.

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule itaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais– TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(h) Kutunza mali za UMMA.
(i) Kuepuka mapambo kama vile mikufu, hereni, rangi za kucha, lipstick, wanja n.k.
(j) Nywele lazima ziwe fupi, kusuka hakuruhusiwi

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

1. Wizi.
2. Uasherati na ushoga.
3. Ubakaji.
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocain, mirungi, kubeli nk.
5. Kupigana au kupiga.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya UMMA.
7. Kudharau bendera ya Taifa.
8. Kuwa mjamzito, kupata mimba au kusababisha ujauzito.
9. Kutoa mimba.
10. Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa watu au shule.
11. Kukataa adhabu kwa makusudi.
12. Kuwa na simu ya mkononi.

4:0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI WAKATI WA KURIPOTI.

(a) Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical Examination Form**)** ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali tu. (***HOSPITAL YA TARIME MJI-BOMANI). Hakikisha wakati wa kuripoti shuleni unakuja na fomu hii ikiambatanishwa na risiti halali ya malipo ya Serikali.***
(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
(d) Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
(e) Passport size nne za mwanafunzi.
(f) Jalada **(spring file)** la kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi.

Tafadhali soma kwa makini maelezo na maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Nakutakia maandalizi mema.

_____
Chacha Nchagwa
(Mkuu Wa Shule)

SHULE YA SEKONDARI TURWA.
FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI.
KUKUBALIANA NA SHERIA ZA SHULE.

1. **TAARIFA ZA MWANAFUNZ**I
   a) Jina kamili la Mwanafunzi……

b) Tarehe ya kuzaliwa……
c) Mahali anapoishi (Mtaa na Kata)……
d) Uraia; MTANZANIA/SI MTANZANIA……
e) Shule ya msingi aliyotoka ……

2. **TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**.

a) Jina la Mzazi/Mlezi……'……
b) Kazi ya Mzazi/Mlezi ……
c) Anuani ya Mzazi/Mlezi ……
d) Mahali anapoishi (Mtaa/Kata)……
e) Namba ya simu……
f) Ndugu/Jamaa wa karibu wa Mwanafunzi. (Jaza jedwali lifuatalo).

Na	Jina la ndugu/ Jamaa	anapoishi	uhusiano	Namba ya simu

3. AHADI/ KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi …… nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote ya kujiunga na shule ya Sekondari Turwa na nimekubali kuipokea nafasi niliyopewa. Ninaahidi kufuata maelekezo yote, sheria na taratibu za shule. Sitashiriki wala kujihusisha na migomo, fujo wala makosa ya jinai. Endapo nitakiuka kiapo hiki uongozi wa shule uchukue hatua za kinidhamu dhidi yangu.

Sahihi …… Tarehe ……

4. AHADI YA MZAZI/ MLEZI.

Mimi ..... mzazi/mlezi wa mwanafunzi ninakiri kukubaliana na sheria za shule, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule, niko tayari kupokea uamuzi utakaotolewa na shule endapo mwanafunzi atavunja sheria, kanuni na taratibu za shule. Pia ninaahidi kushirikiana kwa karibu na uongozi wa shule katika malezi ya mwanangu muda wote wa masomo yake ikiwa ni pamoja na kufuatilia maendeleo yake kitaaluma. Nitampatia mahitaji yote muhimu kama uongozi wa shule utakavyokuwa ukielekeza.

Sahihi ..... Tarehe .....

Fomu hii itasainiwa siku ya mwanafunzi kuripoti shuleni.

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINSTRATION AND LOCAL GOVERNMENT.

MEDICAL EXAMINATION FORM.

Student's full Name .....

Age ..... Height (In Cms) ..... Weight.....

1. Blood court (Red and White).....
2. Stool Examination.....
3. Urine Analysis.....
4. Syphilis and other V.D.....
5. T.B and Leprosy Test.....
6. Eye Test.....
7. Ears Test.....
8. Chest Test.....
9. Abdominal Test.....
10. Plano Test (Girls).....
11. Spleen.....

Additional Information E.g Physical Defects of Impairments Infection Chronic or Family Disease (e.g. Sickle cell) Inability to eat certain foods Etc.

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

.....
.....
.....
.....
.....
.....

I certify that the above named student is Fit/Unfit to pursue Secondary Education as started above.

Signature .....
Designation .....
Station .....
Date .....